**102/1 KISWAHILI (*Insha*) (2018) KCSE *Trial Exam MWONGOZO***

***Mwongozo wa kusahihisha swali la kwanza***

1. Majibu

Mwanafunzi azingatie mtindo wa barua ya kirafiki(kuwe na anwani moja)
Aeleze akitumia mtindo wa wima au mlazo
Ataje hoja zifuatazo kwa mtiririko

- Maamkuzi
- Azingatie hoja hizi
  - ✓ Kuelimisha
  - ✓ Kushauri
  - ✓ Kuburudisha
  - ✓ Kukuza lugha
  - ✓ Kukuza na kuhifadhi utamaduni
  - ✓ Njia ya ajira
  - ✓ Umoja
  - ✓ Ulumbi
  - ✓ Kuinua uchumi wa taifa
  - ✓ Nidhamu

Hoja hizi zitolewe na mifano halisi (insha iwe na maneno 400)
Kuwe na jina la mwandishi na sahihi

2. SWALI LA 2

- Hii ni insha ya mjadala
- Mtahiniwa aunge au apinge
- Pia anaweza kufanya yote mawili kisha atoe uamuzi mwishoni

Hoja za kuunga

- Umma uhamasishwe kufanya kazi kwa bidii
- Ufisadi ukomeshwe
- Wito wa kusaidiana uendelezwe
- Nafasi za kazi zibuniwe
- Mikopo kwa wafanya biashara
- Masharti ya kuanzisha biashara/ uwekezaji yalegezwe n.k.

Hoja za kupinga

- Ni vigumu kuwa na usawa
- Binadamu ni mwovu kimaumbile lazima atamdhulumu mwenzake
- Itachukua muda mrefu kuziba pengo baina ya maskini na matajiri n.k.

3. Methali: Badiliko kwa mjukuu huanza na babu

Maana: Jambo linalotarajiwa kubadilika/ kuwa bora mbeleni huanza kushughulikiwa mapema/ sasa

Matumizi: Kuwatahadharisha wanaosubiri hadi wakati wa mwisho kuanza kulishughulikia jambo – matokeo hayawi mazuri.

Taribihi:

i) Mtahini asimulie kisa/visa vinavyooana na matumizi ya methali.
ii) Si lazima afafanue maana ya methali
iii) Mwishoni aonyeshe funzo lialotokana na kisa/ visa alivyoandika.

4. Mwanafunzi ni lazima atumie mbinu rejeshi ili kutuonyesha kitendo alichokifanya cha kumfedhehesha babake.

Kisa kionyeshe kuwa alikuwa amekanywa lakini hakusikia na kwa hivyo kurudia kitendo alichokuwa amekanywa.

Atuonyeshe damu iliyokuwa ikimtoka ilisababishwa na nini.

Asipotumia mbinu rejeshi amepotoka na asituzwe juu ya alama tatu.

Asipotuonyesha kuwa alikuwa amekanywa na sababu za kutokwa na damu amepungukiwa na asipitishe alama 10